SHULE YA UPILI YA_____

JINA……

NAMBARI YAKO……KIDATO……..

MKONDO……..TAREHE……..

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA

KISWAHIILI

102/2

FEBRUARI/MACHI 2021

MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA DIRA 26

KIDATO CHA TATU

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA

MAAGIZO

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali yote.
(d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
(g) Karatasi hii ina kurasa NNE zilizopigwa chapa.
(h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	40	
3	15	
4	10	
JUMLA	**80**	

UFAHAMU ALAMA 15

Nani kasema mapenzi ni *pweleo* la *tamasha?* Kama mtu hajui mapenzi ni nini mapenzi, akamuulize Dadi *mchuuza samaki*. Naye kwa ulemavu wake wa mapenzi, angesita kutamka kinywa wazifasili ya mapenzi. Labda rohoni mwake tu angeungama kwamba mapenzi ni mateso, ni utumwa, ni ukandamizaji, ni udunishwaji, ni *ushabiki* usio na maana. Kwa ufupi, ni ugonjwa usio na dawa!

****

Mwanzoni, bila ya shaka, mambo hayakufikia kiasi hicho. Pale alipokuwa kufa na kupona akimtafuta Kidawa. Alipokuwa *kiguu na njia* akimwinda kama kunguru mwerevu, moyoni mwake alidhani anafuata nyuki apate kula asali. Ajabu lakini, kwa nini misumari ya nyuki inamuuma sasa ila si wakati ule wa tamaa ya ushindi ilipokuwa mbali, mbingu na ardhi?

Wakati wa siku zile ngumu yeye alipotembea ardhini, Kidawa aliruka hewani. Alipomtandiliza, Kidawa alimwambaa Dadi kama mgonjwa wa tauni. Ilipotokezea kugongana naye ghafla njiani, Kidawa alibirua midomo kumbeza mwindaji wake. Huyo bibiye akakupuka ili kumpa mgongo Dadi. Naye Dadi akafahamu kuwa Kidawa akijenga ukuta makusudi kukata mawasiliano baina yao. Lakini Dadi aliyeyahamu sana mawasiliano hayo, kwa bahati mbaya alimkuta kidawa kila siku anajitia ububu ingawa mdomo wake hauna kizibo chochote cha meno.

***

Hata hivyo, mambo ya Mungu ni mengi, na pia yana miujiza. Siku moja, hata haijulikani kwa nini, Dadi alimwona Kidawa anamjia yeye kama vile alikuwa akilipuka moto mwili mzima, na yeye Dadi akageuka maji ya kuuzima moto huo.

"Bwana wewe unataka mapenzi utayaweza?" Kidawa alimkabili Dadi kinaganaga huku kaweka mikono kiunoni, huku akihisi kuwa Kidawa hivyo ndivyo anavyotakiwa afanye mwanamke wa kisasa.

Dadi alishangaa kwanza. Nusu kajaa kutoamini, nusu furaha. Alishangaa kwa sababu hakujua apite wapi. Siku zote yeye ndiye aliyemzingia Kidawa lakini leo yeye ndiye aliyezingiwa na Kidawa. Si kwa ule mwili mkuza wa Kidawa, bali kwa yale maneno yake ya ajabu. Tuseme nini? Kidawa ameushatuliza moyo wake? Tuseme ameshasalimu amri na kuamua? Aaaa, Dadi hakujongea kulipa muda suala la Kidawa, asije akanyang'anywa tonge mkononi. Akajikuta anaibuka tu, hata haijulikani kutoka wapi, kujibu swali aliloulizwa.

‘’Hata mapenzi yako yawe mazito namna gani Kidawa, ni bora kuliko kasoro ya mapenzi yako. Wewe kwangu si Kidawa jina tu, bali Kidawa dawa ya ugonjwa wangu!” alijibu Dadi huku sauti imekunywa mtetemo wa wasiwasi maana hakuamini. Kusema kweli, nani angeamini? Baada ya visa vyote vile Dadi alivyofanyiwa, nani angeamini?

‘’Sikiliza,” Kidawa alitia maneno yake breki ya kumchuja Dadi kwa kituo.

Lakini kidawa hakuwa na haja ya kumzindua Dadi asikilize kwa makini. Wakakti huu masikio ya Dadi yalikuwa wazi kama anga lote la dunia. Yalikuwa wazi kungojea shuruti za Kidawa ziibuke kule mbali siku zote zilikojificha. Mbali ardhi ya saba nafsi inakoficha mambo!

‘’Sikiliza Dadi! Mimi nimefuatwa na wanaume wengi walionitaka uchumba. Waliosoma na wasiosoma. Wenye uwezo na wasio nao. Lakini nimewapeperusha wote nje ya unyumba na ndoa. Wewe nimekupa mitihani mingi, na naona umeona umefaulu. Nimekupima na kukuona mtu wa maana. Ila tu, Zaidi ya hayo, nataka ujue kuwa mimi ni mwanamke wa kisasa, na mwanamke wa kisasa hutafuta mwanamme wa kisasa, mwenye mapenzi ya kisasa. Na mapenzi ya kisasa yana shuruti za kisasa. Kwa hivyo, ukitaka kunioa, lazima ufanye wajibu wa kisasa kwa mimi nitaakayekuwa mkeo wa kisasa.”

Hili neno kisasa Dadi hakulifahamu maana yake hata kidogo! Na si ajabu. Maneno mengi ya lugha ya siku hizi huwa hayana maana wazi kiasi hicho. Basi tu hapa, jinsi neno hilo lilivyotumiwa na Kidawa, lilitokezea kugonga vizuri masikioni mwa Dadi. Liligonga kimziki kwa urari wa vina na mizani. Na lilipogonga, lilimwingia Dadi moyoni mwake kwa ladha ya ajabu!

‘’Mimi ni muuza samaki tu, kamwe silingani na wewe kwa elimu uliyonayo ya madarasa kumi na mawili. Hata hivyo, nimezaliwa hapa jijini. Nikakulia katika nyakati hizi hizi za kisasa. Kwa hivyo naujua usasa vizuri. Na nitakuwa tayari kuutekeleza kwako kama unavyotaka wewe mwanamke wa kisasa.”

Kidawa alitabasamu kidogo kwa kauli ya Dadi. Dadi naye akaona kama vile mbele yake nyota ya jaha imechomoza. Sauti ya ndani ya nafsi yake ikamwambia: ‘Hapana lisilowezekana Dadi. Hapana gumu lisilogeuzika kuwa laini.’ Dadi akatabasamu pia.

Muda ukapita kidogo halafu mara akamsikia Kidawa akinena, ‘’Niko tayari basi kuolewa na wewe, njoo unipose kwetu wakati wowote ule. Ninakungojea.”

Unaweza kukisia jinsi hisia za furaha zilivyokuja ghafla kumjaa tele pale kifuani pake Dadi. Zilimjaa na kumsonga mpaka akawa hawezi kuzizuia tena. Kila siku sasa Dadi akawa anapita njiani kuzimwaga nje hisia za furaha kwa

kukenua, kutabasamu na kucheka hasi pasina kuweko wazi kitu cha kuchekesha. Mpaka jamaa wakamgeuza jina, wakamwita Dadi Kichekaheka.

Pamoja na hayo yote, Dadi kamwe hakufahamu uzito wa maneno yale ya Kidaw yaliyotonewa kama kito chenye thamani neno "kisasa" hatua kwa hatua, kipembe baada ya kipembe. Kwa sababu hakufahamu maana wala uzito wa maneno yale, hakuweza kuyazingatia vyema. Alijaribu kuyapinduapindua, kuyapekuapekua na kuyabiruabirua ili apateasili iliyomfanya afungike na maneno yale ya masharti tokea wakati ule yaliposhurutishwa na Kidawa. Ilikuwa kama vile hatia saini ya kukubali kutiwa kitanzi bila ya kutambua vipengele vya sheria za utiaji huo wa kitanzi.

Sasa kwa jinsi ya ule ukweli kwamba keshamtia Kidawa mikononi mwake, na kwa jinsi mapenzi yake Dadi yalivyokamilishwa na uamuzi wa Kidawa, alipoondoka pale tu, baada ya kufunguliwa peto za ndani za moyo wa Kidawa, Dadi alidhani kwamba yeye ndiye atakayeumiliki na kuutawala uwanja wa mapenzi ya Kidawa, kwani yeye ndiye aliyeshinda miongoni mwa wengi waliomtaka Kidawa. Wengi walikosa kuuzuru uwanja wa Kidawa wa mapenzi, seuze kuutawala.

Lakini wapi? Kakosea Dadi kufikiri hivyo. Kakosea sana.

MASWALI

a. Kipe kifungu hiki kichwa mwafaka kwa kurejelea wahusika. alama 1

b. Toa kijelezi cha mapenzi kulingana na Dadi. alama 2

c. Fafanua sifa mbili za Kidawa kwa kurejelea kifungu hiki. alama 4

d. Mwandishi wa kifungu hiki amedhihirisha pakubwa kwamba ana umilisi wa Lugha ya Kiswahili. thibitisha kwa hoja tatu kutoka katika kifungu hiki. alama 6

e. Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kwa mujibu wa kifungu:
   i. Pweleo la tamasha

   ii. Kiguu na njia

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Ponografia ni tendo, maandishi, picha au mchoro unaoonyesha au kueleza uchi wa mtu au vitendo vya ngono kwa ajili ya kuchochea ashiki ya kuifanya. Mambo haya machafu huwasilishwa ana kwa ana kupitia sinema, video, magazeti, vitabu, muziki, televisheni. DVD, n.k.

Ponorafia imekuwepo tangu jadi, hasa katika nchi za magharibi. Lakini sasa limekuwa tatizo sugu. Hii ni kwa sababu imeenea ulimwenguni kote mithili ya moto katika mbuga wakati wa kiangazi. Uenezi umechangiwa na mambo kadha wa kadha. Mchango mkubwa zaidi umetokana na kuimarika kwa vyombo vya teknolojia ya habari na mawasiliano. Matumizi ya tarakilishi, mdahilishi na viungambali vya picha yamesambaza ponografia ilivyoanza.

Hata hivyo, hubuniwa au kutengenezwa na makundi mbali mbali ya watu. Miongoni mwa hawa ni watu wasiojali maadili. Pili, kuna wale wenye matatizo ya kisaikolojia na kijamii. Wao hutengeneza na kueneza uchafu huu kwa lengo la ama kuvuruga maadili katika jamii au kuchukiza wanajamii waadilifu. Kundi lingine ni lile la wanaoichukulia ponografia kama nyenzo ya kutosheleza ashiki zao. Hivi sasa, kundi kubwa ni lile la wanotumia matusi haya kama njia ya kuchuma. Kwa mfano, wanamziki ambao hutumia ponografia kuvutia wateja na hivyo kuzidisha mauzo yao.

Kushamiri kwa wimbi na uonyeshaji ponografia kuna athari kubwa kwa jamii na hasa watoto. Ingawa watu wengine hudai picha hizi haziwaathiri, upo ushahidi kuonyesha kuwa wanaotazama picha za ngono hupata matatizo. Lazima ieleweke kuwa kinachoonekana na jicho au kusikika kwa sikio huathiri fikira au hisia. Picha za matusi zinachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu akili. Badala ya kuzingatia mambo muhimu kama masomo watu huanza kutafakari mambo machafu.

Vijana wengi ni kama bendera. Hivyo basi huanza kuiga wanayoyaona na kusikia. Hili ni tatizo linalowafanya kuacha mkondo wa maadili. Kutokana na uchafu huu, watu wengi hushawishiwa kuingilia shughuli za ngono mapema kabla hawajakomaa kimwili, kiakili na kihisia. Matokeo yake ni mengi. Haya ni pamoja na ukahaba, utendaji mbaya shuleni, mahudhurio mabaya darasani na mimba zisizotarajiwa. Vijana wengi huacha shule kabisa. Wengine nao huambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo huwaletea mauti.

Inasemekana kuwa akili za binadamu hunata zaidi mambo yanayowasilishwa kwa picha. Si ajabu vijana huyadumisha matusi haya katika kumbukumbu zao na kuyasanya sehemu ya maisha yao. Wengi huanza kuandama tabia mbovu kama ushoga, ubasha na usagaji. Kuna wale ambao huanza kujichua. Kujichua ni hali ya mwanamke au mwanaume kumaliza haja za kimaumbile bila kufanya mapenzi na mtu mwingine. Ponografia imechangia pakubwa kuenea kwa haya.

Jambo hili limegeuza mielekeo ya vijana. Wanaiga mitindo mibaya ya mavazi yanayoanika uchi wao. Hali kadhalika, huiga lugha, ishara na miondoko inayohusiana na ngono. Yote haya yanapingana na desturi za Mwafrika. Si ajabu visa vya ubakaji vinaongezeka kila kukuchapo.

Utazamaji wa picha chafu aghalabu huandamana na maovu mengine kama unywaji pombe, matumizi ya dawa za kulevya, uvutaji sigara na utumiaji wa dawa za kuchochea uchu wa ngono. Mambo haya huwapa vijana kutazama tabia za unyama.

Jambo hatari ni kuwa kuendelea kutazama picha hizi huzifanya nishai na hisia za watu kuwa butu, yaani huondoa makali. Hata katika utu uzima,

mtu atapoteza mhemko wa kawaida na kugeuzwa kuwa mtegemezi wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mijini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na maenezi haya yasio na kizuizi.

Jambo la kwanza ni kuongeza ufahamu wa umma wote kuhusu uovu wa picha hizi. Kwa namna hii itawezekana kupunguza mahitaji na uuzaji wa ponografia. Tatizo hili linaenea kwa vishindo mijini na vijijini. Ipo haja ya dharura kuikinga jamii kutokana na maenezi haya yasiyo na kizuizi.
Tatizo la kuenea kwu ponografia limeendelea kuwepo kwa sababu ya udhaifu wa sheria. Kilichoko basi ni kuweka sheria za kuzuia utengenezaji wa upujufu huu. Kuambatana na haya, hatua kali zichukuliwe kwa wanaovunja sheria hizi. Hali kadhalika, ushirikiano wa karibu baina ya wadau uimarishwe katika ulimwengu mzima. Serikali na wanaohusika wakabiliwe ipasavyo. Jamii ingependa kuona michakato ya kuharamisha utengenezaji, usambazaji na utangazaji wa ponografia ikiwekwa.

Wazazi nao wasijipweteke tu bali nao wasaidie. Ni muhimu washikilie kwa sharti juhudi zao za kuwaelekeza na kuwashauri watoto kuzingatia uongofu na kukwepa picha hizi najisi. Watoto lazima waeleweshwe kuwa haifai kutazama picha au michoro michafu. Itikadi na imani za kidini na utamaduni wa Kiafrika unakataza vikali mtu kuona uchi wa mtu mwingine. Matokeo ya kuasi makatazo haya yana madhara makubwa kwa watu na jamii.

<u>Maswali</u>

a) Fupisha ujumbe wa aya ya pili na ya tatu kwa maneno 20 – 25

(alama 6, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Nakala safi

b) Kwa kutumia maneno 55 – 60, eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika aya ya nne hadi ya tisa kuhusu athari za ponografia . (alama 9, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Nakala safi

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Taja sauti mbili zinazotamkiwa kwenye kaakaa laini (alama 1)

b) Eleza tofauti za sentensi zifuatazo (alama 2)

i) Amerudi shuleni!

ii) Amerudi shuleni.

c) Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mstari.

i) Afisa mkuu anafuata sharia sembuse wewe. (alama 1)

ii) Ameenda huko mbali <u>sokoni</u> (alama 1)

d) Tambua aina ya vihusishi katika sentensi zifuatazo

i) Jumba alifuatalo li mbele ya msikiti wa Musa (alama 1)

ii) Kisiwa cha Ginigi kimekauka (alama 1)

e) Tambua hali katika sentensi ifuatayo.

Vyungu vya aina hii vyafinyangwa na huyu. (alama 1)

f) Toa maana mbili za neno lifuatalo (alama 2)

Somo

g) Kanusha

Mama alimwambia Sipo alime haraka (alama 1)

h) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano

i) La (Kutendeshwa) (alama 1)

ii) -Ja (Kutendea) (alama 1)

i) Andika katika hali ya wastani umoja
Kigombe kile kiliumia kikwato (alama 2)

j) Akifisha sentensi ifuatayo.
Je kuna manusura wowote yeye alitaka kujua. (alama 2)

k)

i) Eleza maana ya kirai (alama 1)

ii) Onyesha aina mbili za virai katika sentensi ifuatayo.
Nilimpata akilalama ndani ya darasa (alama 2)

l) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.
Mwelekezi wake alimwambia kuwa angeweza kuwa mwindaji mashuhuri ikiwa angeyafuata mashauri yake. (alama 2)

m) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mstari.
Mtoto mmoja aliyekuwa mgonjwa sana alitibiwa jana. (alama 3)

n) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia “o” rejeshi
Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo (alama 2)

o) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo
Wauguzi shupavu wamenununuliwa vifaa vya kufanyia kazi (alama 2)

p) Tumia kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi katika sentensi (alama 2)

q) Onyesha viambishi katika fungutenzi hili (alama 2)
Anasomeshwa

r) Eleza matumizi ya “na” kama aina ya neno. (alama 2)

s) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo (alama 2)

i) Tubu

ii) –fa

t) Weka vitenzi hivi katika hali ya kuamrisha kulingana na maelezo katika mabano (alama 2)

i) omba (umoja)

ii) lima (wingi)

u) Nini maana ya nahau “kula mtu roho” (alama 1)

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

“Toa zote mpaka senti ya mwisho!Unanisikia,chapuchapu au nikuset.

a. Hii ni sajili gani? Toa sababu. (alama 2)

b. Eleza sifa NNE za sajili hii (alama 8)